

## **BILIONI TATU MILIONI MIAMOJA TISINI ZAJENGA HOSPITALI YA WILAYA BUKOBA**



Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliwahi kusema “Mtu hujiimarisha anapokua au anapokuwa na kipato cha kutosha kujipatia mazingira bora kwa ajili yake yeye mwenyewe na familia yake; haimariki endapo atapewa vitu hivyo na mtu mwingine”

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imedhihirisha kauli hiyo ya mwalimu Nyerere kwa kuamua kutumia fedha zake kujenga hospitali, vituo vya afya na zahanati katika Halmashauri zote nchini ili kuhakikisha kwamba wananchi wa Tanzania wanapata huduma bora za afya na kuendelea kujenga taifa imara maana mwili usipokuwa na afya njema mtu hawezi kuwa na akili safi na imara.

Halmashauri ya Wilaya Bukoba ikiwa ni moja kati ya Halmashauri 195 zilizomo nchini nayo imefikiwa na jitihada hizo za serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo mnamo mwaka 2019 ilipokea jumla

ya shilingi bilioni moja milioni mia tano (1.5 Billion) kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Hospitali ya Wilaya katika kijiji Bujunangoma kata Kemondo. Hii ikawa ndio awamu ya kwanza ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya Bukoba ambapo majengo saba ambayo ni jengo la utawala, jengo la wagonjwa ya nje (OPD), jengo la maabara, jengo la mionzi, jengo la stoo ya dawa, jengo la kufulia na jengo la huduma ya mama na mtoto yalijengwa.



Kama ilivyo ada, safari moja huanzisha nyingine hivyo basi mnamo mwaka 2020 ujenzi wa hospitali hiyo uliingia katika awamu ya pili ambapo Halmashauri ilipokea jumla ya shilingi milioni mia tatu (300,000,000/=) kwa ajili ya kujenga kichomea taka (incinerator) na mifumo ya maji safi na maji taka na kazi ikakamilika hatimaye baadhi ya huduma za afya msingi kama vile huduma ya mama na mtoto na huduma za wagonjwa wa nje zikaanza kutolewa katika hospitali hiyo.

Kwa kuwa lengo la Serikali ni kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora na kamilifu za afya kwa wagonjwa ya nje na wa ndani pia mwaka huo huo wa 2020 awamu ya tatu ya ujenzi wa Hospitali hiyo ilianza kwa Halmashauri kupokea jumla ya shilingi milioni mia tano (500,000,000/=) kwa ajili ya ujenzi wa wodi tatu ambazo ni wodi ya wanaume, ya wanawake na ya watoto ili hatimaye huduma za wagonjwa wa ndani ambazo huhusisha kulaza wagonjwa hospitalini hapo zianze kutolewa.



Katika mwaka wa fedha 2021/2022 ujenzi uliingia katika awamu ya nne kwa kupokea jumla ya shilingi milioni mia nane kutoka serikali kuu pia kwa ajili ya ujenzi wa majengo manne ambayo ni jengo la upasuaji, wodi ya upasuaji ya wanawake, wodi ya upasuaji ya wanaume na nyumba ya kuhifadhia maiti (mortuary).

Mara nyingi watu husema ukijipenda na wengine watakupenda na ukijisaidia na wengine watakusaidia hivyo serikali ya jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia shirika la fedha la Dunia (IMF) ilileta jumla ya shilingi milioni tisini kwa ajili ya ujenzi wa nyumba tatu katika moja za watumishi katika Hospitali hiyo ya Wilaya jambo ambalo kwa kweli litarahisisha utoaji wa huduma za afya kwa wananchi na hasa nyakati za usiku maana watumishi watakuwa karibu na hospitali.



Ili hospitali iweze kukamilika inahitaji kuwa na majengo ishirini na mbili na mpaka sasa inayo majengo kumi na nne. Pia inahitaji kuwa na watumishi mia mbili wakiwemo madereva na wafanya usafi na mpaka sasa ina jumla ya watumishi kumi na sita wa kada mbalimbali za afya na hivi karibuni imepokea waajiriwa wengine wapya kumi na tano wakada mbalimbali za afya ambao endapo wataripoti wote kazini basi hospitali itakuwa na jumla ya watumishi thelathini na moja.